

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Anuani ya simu "ELIMU"
Simu: 026 296 35 33
Barua pepe: info@moe.go.tz
Tovuti: www.moe.go.tz



Mji wa Serikali,
Eneo la Mtumba,
Mtaa wa Afya,
S. L. P. 10,
40479 DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

13 FEBRUARI, 2023

**ZUIO LA VITABU AMBAVYO MAUDHUI YAKE HAYAENDANI NA MILA, DESTURI
NA UTAMADUNI WA MTANZANIA KUTUMIKA KATIKA SHULE ZOTE**

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Profesa Adolf Mkenda amepiga marufuku matumizi ya vitabu 16 vilivygundulika kuwa na maudhui yanayokinzana na Mila, Desturi na Utamaduni wa Mtanzania katika shule zote nchini kuanzia tarehe 13 Febrauri, 2023.

2. Taarifa hiyo imetolewa Jijini Dodoma na Profesa Adolf Mkenda alipozungumza na Waandishi wa Habari. Amepiga marufuku matumizi ya vitabu hivyo kupitia **mamlaka aliyopewa chini ya Kifungu cha 59 cha Sheria ya Elimu Sura ya 353 na kusisitiza kuwa zoezi la kufuatilia maudhui yaliyo katika vitabu vilivyopo katika shule ni endelevu**. Vitabu vilivyopigwa marufuku ni vifuatavyo:-

- i. Diary of a Wimpy Kid
- ii. Diary of a Wimpy Kid -Rodrick Rules.
- iii. Diary of a Wimpy Kid-The Last Straw
- iv. Diary of a Wimpy Kid-Dog Days
- v. Diary of a Wimpy Kid-The Ugly Truth
- vi. Diary of a Wimpy Kid-Cabin Fever
- vii. Diary of a Wimpy Kid-The Third Wheel
- viii. Diary of a Wimpy Kid-Hard Luck
- ix. Diary of a Wimpy Kid-The Long Haul
- x. Diary of a Wimpy Kid-Old School
- xi. Diary of a Wimpy Kid-Double Down
- xii. Diary of a Wimpy Kid-The Gateway

- xiii. Diary of a Wimpy Kid- Diper Overlude
- xiv. Is for TANSGENDER (you know best who you are!)
- xv. Is for LGBTQIA (find the words that make you you)
- xvi. Sex Education a Guide to Life

3. Waziri amezitaka shule zote za Awali, Msingi na Sekondari zilizosajiliwa na zinazotoa huduma ya elimu ndani ya Tanzania, zinazotumia mtaala wa ndani ya nchi au mtaala wowote wa kimataifa, kutekeleza masharti yote yaliyoainishwa katika **Waraka wa Elimu Na. 4 wa Mwaka 2014.**

4. Waraka wa Elimu Na.4 wa Mwaka 2014 pamoja na mambo mengine, unatoa muongozo wa Vitabu vya Ziada na Kiada vinavyotumika katika shule zilizosajiliwa nchini (zinazotumia mtaala wa ndani na zile zinazotumia mtaala wa kimataifa), kuwa na maudhui yanayoendana na Mila, Desturi na Utamaduni wa Mtanzania.

5. Aidha, shule zote zinakumbushwa kuzingatia kuwa Vitabu vyote vya Ziada (supplementary books) ambavyo huandaliwa na waandishi/wachapaji binafsi vinatakiwa kuwa na idhini/ithibati ya ubora inayotolewa na Kamishna wa Elimu. Kwenda kinyume na muongozo huo ni kukiuka masharti ya usajili wa shule na hatua stahiki za kisheria zitachukuliwa endapo itabainika kuna shule zinaendelea au zinatumia vitabu ambavyo havijapata idhini/ithibati.

6. Ametoa wito kwa wazazi, walimu na jamii kwa ujumla kukagua maudhui ya vitabu, picha, video na maudhui mengine ya kimtandao yanayotumiwa na watoto/wanafunzi ili kuhakikisha maudhui yake yanaendana na mila, desturi na utamaduni na hayaathiri makuzi.

7. Wizara itaendelea kufuatilia kwa karibu vitabu vinavyotumika katika shule na Taasisi za Elimu na itachukua hatua stahiki kwa shule au taasisi itakayoruhusu matumizi ya vitabu vyenye maudhui potofu.

8. Waziri ametoa rai kwa umma kutoa taarifa iwapo watakuta vitabu vilivyopigwa marufuku au vingine vya aina vyenye maudhui potofu katika maeneo ya shule na Taasisi za Elimu kupitia namba za simu **0262160270 simu ya mezani na 0737962965**, kituo cha Huduma kwa Mteja Wizara ya Elimu , Syansi na Teknolojia.



IMETOLEWA NA

KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI